

MFANO WA UWEKEZAJI IKIWA FAIDA NI 13.5% KWA MWAKA

UWEKEZAJI KILA MWEZI	MWAKA WA KWANZA	MWAKA WA PILI	MWAKA WA TATU	MWAKA WA NNE	MWAKA WA TANO
50,000	638,553	1,368,850	2,204,072	3,159,294	4,251,756
100,000	1,277,106	2,737,700	4,408,143	6,318,587	8,503,513
250,000	3,192,765	6,844,249	11,020,359	15,796,468	21,258,782
500,000	6,385,531	13,688,499	22,040,717	31,592,935	42,517,564
1,000,000	12,771,061	27,376,998	44,081,434	63,185,871	85,035,127

MAWAKALA WETU

- Mawakala wote wa soko la hisa la Dar es salaam.
- Matawi yote ya benki ya NBC, EXIM, AZANIA, CRDB, NMB, MWANGA HAKIKA BANK na COOP BANK.

UWEKEZAJI KATIKA MIFUKO YA PAMOJA INAVYOFANYA KAZI

01



Mwekezaji
Anawekeza

02



APeF Inawekeza
Kwa Niaba

03



Mapato
Yanzalishwa

04



Mwekezaji
Anapokea Faida



WASILIANA NASI

Namba ya simu ya bure
0800 11 1234

Simu:
+255 22 2600166

Barua pepe:
apef@apef.co.tz

Tovuti:
www.apef.co.tz

LinkedIn:
Africa Pension Fund

Facebook:
apeftanzania

Instagram:
apeftanzania

Youtube:
apeftanzania

Anuani:
Africa Pension Fund Limited
Ghorofa ya pili, Jengo la Tawi la
Benki ya Exim - Masaki, Barabara
ya 153, Haile Selassie, Dar es salaam



SIKANI
HAPA KWA
TAARIFA ZAIDI

Ziada
FUND

MFUKO WA ZIADA

Unastahili Zaidi

MFUKO WA ZIADA NI NINI?

Ziada ni mfuko wa uwekezaji wa pamoja unaowekeza kwenye masoko ya fedha na dhamana. Mwekezaji anapata faida za uwekezaji na faida za bima ya maisha.

Bima ya maisha kwa mwekezaji itakuwa na kiwango cha juu cha 50% ya thamani halisi ya vipande, ambayo huanzia TZS 250,000 hadi TZS 100,000,000.

DHUMUNI LA MFUKO

Kuwapa fursa wawekezaji kuwekeza katika mfuko ulio wazi kwa ajili ya, kuwekeza fedha zao kwa kipindi cha muda mfupi au mrefu huku, wakikuza akiba na mitaji yao katika ukuaji wa ushindani.

UPEKEE WA MFUKO HUU

Mfuko wa Ziada unatoa usalama kwa wawekezaji wake kutokana na, kufanya uwekezaji anuai (mseto) ili kuhakikisha upatikanaji wa fedha, kukuzwa kwa mitaji na pia kuwapa wawekezaji manufaa ya bima ya maisha na ulemavu wa kudumu.

NANI ANAWEZA KUWEKEZA

Mfuko uko wazi kwa Mtanzania aliye ndani au nje ya nchi. Watu binafsi na wawekezaji wasio watu binafsi kama mabenki/mashirika, taasisi za serikali zinaweza pia kuwekeza katika mfuko huu.

KIASI CHA UWEKEZAJI

Mwekezaji anaanza kuwekeza kwa kiwango cha chini kikiwa ni TZS 50,000 na kiwango ongezeko kikiwa kuanzia TZS 10,000. Kima cha chini cha mwekezaji kufaidika na bima ya maisha ni TZS 250,000. Mfuko huu hauna ukomo wa juu wa kiasi cha kuwekeza na uwekezaji unianza mara baada ya kufungua akaunti ya Ziada.

JINSI YA KUJIUNGA

Mwekezaji anaweza kujiunga na mfuko wa Ziada kwa kutumia njia zifuatazo :

● Msimbo (USSD)

Kwa watumiaji wasio na “Smartphone” piga *150*74# kwenye simu yoyote ya mkononi na fuata hatua rahisi za kujiunga na mfuko.

● Programu ya Tumizi (App)

Pakua app ya APeF kupitia Google Play Store au Apple Store .

Baada ya kupakua programu hiyo, fuata maelekezo ya kujisajili ili kutengeneza akaunti yako na kuanza kuwekeza.

● Tovuti

Tembelea tovuti yetu ya apef.apef.co.tz, jaza taarifa zako na uanze kuwekeza pesa zako.

UZAJI WA VIPANDE

Vipande vitauzwa kila siku ya kazi kuanzia tarehe 26 Januari mpaka 25 Februari 2026 kutokana na thamani yake halisi. Ripoti ya utendaji wa mfuko itatolewa kila wiki.

SERA YA UWEKEZAJI

Mfuko utawekeza kwenye masoko ya fedha na dhamana kwa asilimia mia (100%).

KIGEZO

Hatifungani za serikali za miaka miwili

MIKONDO YA UWEKEZAJI

Hatifungani za serikali za mda mrefu na mfupi, Hatifungani za makampuni na amana za benki.

FAIDA ZA BIMA YA MAISHA

● Iwapo mwekezaji atafariki au atapata ulemavu wa kudumu, mfuko utatoa kiasi cha 50% ya thamani ya uwekezaji wake kama malipo ya bima, pamoja na kiasi chote cha uwekezaji wake. Kwa mfano, ikiwa uwekezaji wake ni TZS Milioni 5, warithi wake (iwapo amefariki) au mwekezaji mwenyewe (iwapo amepata ulemavu) atapokea jumla ya TZS Milioni 7.5

● Msaada wa Mazishi kwa Watoto: Endapo mtoto atafariki, mfuko unatoa msaada wa mazishi kati ya TZS 250,000 hadi TZS 1,000,000, kulingana na thamani ya uwekezaji wako.

USALAMA WA MTAJI

Mfuko huu umeweka kipaumbele kwenye kulinda mtaji wa uwekezaji hivyo kuongeza usalama. Lengo ni kuzalisha faida thabiti kupitia utawanyaji wa uwekezaji katika dhamana mbalimbali.

KWANINI UCHAGUE MFUKO WA ZIADA?

- Usalama-Tunapunguza vihatarishi kwa kufanya uwekezaji wa mseto kwenye Masoko ya fedha na dhamana.
- Ukuzaji wa mitaji - Fedha za wawekezaji zitakuzwa na faida.
- Ukwasi - Wawekezaji watapata fedha zao ndani ya siku tatu za kazi.
- Bima ya maisha - Mfuko unatoa faida ya bima ya maisha na ulemavu wa kudumu.
- Uwazi - Thamani halisi ya vipande na mfuko hutolewa kila siku ya kazi
- Uratibu - Mfuko unaratibiwa na Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana (CMSA)
- Dhamana - Vipande vinaweza kutumika kama dhamana ya mkopo.